# 4th INTERNATIONAL CONFERENCE ON PUBLIC HEALTH IN AFRICA

International CPHIA 2025 Conference on Public Health in Africa

**KUCHUKUA MKONDO WA KUJITEGEMEA ILI KUFANIKISHA UTOAJI WA HUDUMA YA AFYA KWA WOTE NA USALAMA WA AFYA BARANI AFRIKA**

## KUHUSU **CPHIA 2025**

Likiwa limeandaliwa kwa pamoja na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa vya Afrika (Africa Centres for Disease Control and Prevention, Africa CDC) na Serikali ya Afrika Kusini, kwa ushirikiano na Kongamano la 8 la Kila Mwaka la BIO Africa la AfricaBio, kongamano la CPHIA 2025 litaandaliwa chini ya mada "Kuchukua mkondo wa kujitegemea ili kufanikisha utoaji wa huduma ya afya kwa wote na usalama wa afya barani Afrika."

Likiwa linafanyika katika wakati nyeti wa usalama wa afya barani Afrika, kongamano la CPHIA 2025 litaleta pamoja viongozi wa Afrika, wataalamu wa afya ya umma, watetezi na wawakilishi wa jamii ili kuangazia na kuharakisha kuchukuliwa kwa hatua ya kukabiliana na changamoto nyeti za afya na kuwezesha upatikanaji wa mifumo ya afya ya kudumu na inayojitegemea.

Kupitia ajenda ya kina inayojumuisha vikao vya wazi vya kushirikisha vinavyoongozwa na mada na nadharia na mpango wa maonyesho na matukio rasmi ya kando, kongamano la CPHIA litaonyesha suluhu bunifu zinazoongozwa na Afrika zinazotumia teknolojia, ujuzi wa jamii na ushirikiano wa sekta mbalimbali ili kuimarisha ufadhili wa afya, mageuzi katika matibabu ya msingi na utengenezaji wa bidhaa za barani.

Kama kongamano muhimu zaidi la afya ya umma barani, kongamano la CPHIA 2025 linakuza ajenda inayoongozwa na Afrika nje ya kumbi za mikutano na kuchangia katika maamuzi yanayofanywa katika majukwaa makuu ya kimataifa, ikijumuisha G20 nchini Afrika Kusini.

**TAREHE:** 22 hadi 25 Oktoba 2025

**MAHALI:** Durban International Convention Centre, Durban, Afrika Kusini

## AJENDA ZA **KONGAMANO**

**Ajenda ya 1:** Safari ya kujenga usalama wa afya barani Afrika kupitia uwezo wa bara wa kutengeneza bidhaa zote za afya

**Ajenda ya 2:** Kuimarisha hali ya kujitegemea na usalama wa afya kupitia ufadhili bunifu na wa kudumu wa afya katika utoaji wa huduma ya afya kwa wote barani Afrika

**Ajenda ya 3:** Kurejelea huduma ya afya ya msingi ili kuimarisha utoaji wa huduma ya afya kwa wote barani Afrika

**Ajenda ya 4:** Kuwezesha Afrika yenye afya zaidi kupitia ubunifu dijitali na akili unde

**Ajenda ya 5:** Mabadiliko ya hali ya anga na Afya Moja: Kuimarisha usalama wa afya ya Afrika

**Ajenda ya 6:** Wanawake na vijana barani Afrika: Kuendeleza afya na ubunifu

**Ajenda ya 7:** Viwango Vipya katika kukabiliana na magonjwa

**Ajenda ya 8:** Ustahimilivu wa majanga na utayari wa mifumo ya afya katika uzuiaji, uchunguzi na ukabilianaji wa magonjwa ipasavyo barani Afrika

## UNAWEZA KUJIANDIKISHA SASA!

Ili upate maelezo zaidi na kujiandikisha leo, tembelea cphia2025.com
Ukiwa na maswali, tafadhali wasiliana na Usimamizi Mkuu wa CPHIA 2025: CPHIASecretariat@africacdc.org

## WENYEKITI WENZA WA CPHIA 2025

**Profesa Olive Shisana** (Rais, Evidence Based Solutions)
**Profesa Placide Mbala Kingebeni** (Mkurugenzi, Taasisi ya Kitaifa ya Utafiti wa Matibabu na Viumbe Hai (National Institute of Biomedical Research))

AfricaCDC Centres for Disease Control and Prevention | An entity of the African Union | Republic of South Africa | AFRICABIO | BIO Africa Convention

## VIONGOZI WA AJENDA ZA KAMATI YA MPANGO WA KISAYANSI WA CPHIA 2025

| Ajenda | Mwenyekiti mwenza |
|---|---|
| Ajenda ya 1 | **Prof. Abderrahmane Maaroufi**, Mkurugenzi, Institute Pasteur (Taasisi ya Kitaifa ya Afya ya Umma), Moroko |
| | **Bw. Kevin Irandagiye**, Kiongozi wa Mawasiliano wa Ushirikiano wa Utengenezaji wa Chanjo ya Afrika (Partnerships for African Vaccine Manufacturing, PAVM), Africa CDC |
| Ajenda ya 2 | **Prof. Richard Chivaka**, Mwanzilishi na Afisa Mkuu Mtendaji, Spark Health Africa |
| | **Dkt. Maraki Fikre Merid**, Mkurugenzi Msimamizi, CHS Advisory |
| Ajenda ya 3 | **Dkt. Amit Thakker**, Mwenyekiti Mkuu, Africa Health Busines |
| | **Prof. Maha El Rabbat**, Waziri wa Zamani wa Afya na Idadi ya Watu wa Misri na Profesa wa Afya ya Umma, Chuo Kikuu cha Cairo |
| Ajenda ya 4 | **Dkt. Francis Ohanyido**, Mkurugenzi Mkuu Mwanzilishi, Taasisi ya Afya ya Umma ya Afrika Magharibi (West African Institute of Public Health, WAIPH) |
| | **Prof. Otto Chabikuli**, Profesa Mshirika wa Muda, Chuo Kikuu cha Howard |
| Ajenda ya 5 | **Prof. Rashid Ansumana**, Mkuu wa Kitivo, Shule ya Sayansi za Afya ya Jamii, Chuo Kikuu cha Njala |
| | **Dkt. Doris Wangari**, Afisa Mkuu wa Mpango, Sayansi ya Msingi wa Afrika |
| Ajenda ya 6 | **Prof. Nkandu Luo**, Waziri wa Zamani wa Afya wa Zambia na Mwanzilishi, Taasisi ya Afya ya Global One |
| | **Dkt. Kechi Achebe**, Mkurugenzi wa Ofisi ya Afya ya Jumla na VVU (Office of Global Health and HIV, OGHH), Peace Corps |
| Ajenda ya 7 | **Dkt. Awatef Belakhel**, Mtaalamu wa Afya ya Umma na Kiongozi wa Kitengo cha Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza, Wizara ya Afya, Moroko |
| | **Prof. Kaushik Ramaiya**, Daktari Mshauri na Msimamizi Msaidizi wa Matibabu, Hospitali ya Shree Hindu Mandal, Tanzania |
| Ajenda ya 8 | **Dkt. Abel Ntambue**, Mtaalamu wa Magonjwa na mtaalamu katika Afya ya Akina Mama, Watoto Wachanga na Watoto Wadogo (Maternal, Newborn and Child Health, MNCH), Chuo Kikuu cha Lubumbashi, DRC |
| | **Dkt. Peter Elyanu**, Mkurugenzi wa Usalama wa Afya ya Jumla, Chuo cha Baylor College of Medicine Children's Foundation, Uganda |